

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA MAJI



TAARIFA KWA UMMA: WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA RUWASA

Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa (MB), kwa kuzingatia mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Sheria Na.5 ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019, ameteua wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya RUWASA. Hatua hii inakamilisha kuundwa kwa Bodi ya Wakurugenzi ya RUWASA kufuatia kuteuliwa kwa Mwenyekiti wake, Prof. Idrissa Bilali Mshoro, kulikofanywa na Mheshimiwa Rais. Safu kamili ya Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya RUWASA ni kama ifuatavyo:

- | | |
|-----------------------------------|-------------------|
| 1. Prof. Idrissa Bilali Mshoro | Mwenyekiti |
| 2. Eng. Ngwisa Mpembe | Mjumbe |
| 3. Eng. Loishiye Longiteng Ngotee | Mjumbe |
| 4. Eng. Amos William Maganga | Mjumbe |
| 5. Bw. Salehe Njaa | Mjumbe |
| 6. Bi. Grace Chitanda | Mjumbe |
| 7. Eng. Nadhifa Sadik Kemikimba | Mjumbe |
| 8. Prof. Evelyne Isack Mbende | Mjumbe |
| 9. Eng. Clement Lenard Kivegalo | Katibu |

Kuhusu RUWASA

RUWASA ni kifupi cha **Rural Water Supply and Sanitation Agency**, ikiwa ni Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Wakala huyu ana jukumu la kusanifu na kusimamia ujenzi wa miradi ya maji vijijini, na kuhakikisha kuwa huduma ya maji vijijini inawafikia wananchi walio wengi kwa mujibu wa malengo ya kitaifa.

Tunawatachia kila heri Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi katika kutekeleza majukumu yao.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Prof. Kitila Mkumbo".

Prof. Kitila Mkumbo
KATIBU MKUU
30 Septemba, 2019.